Nina Paswa Kuabudu Katika Kanisa Lipi?

na

Jerry McCay

Nina Paswa Kuabudu Katika Kanisa Lipi?

na

Jerry McCay

Novemba 16, 2012

Ninapaswa Kuabudu Katika Kanisa Lipi?

Yohana 14:1-6

Yoh. 14:1-6, "*Msifadhaike mioyoni mwenu mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandali mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia. Tomaso akamwambia Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia? Yesu akamwambia mimi ndimi njia, kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Tukitaka ahadi hii iliyotolewa na Kristo tuitumie, tunapaswa kuamua ni kanisa lipi tunalopaswa kuabudu. Au, ni katika kanisa gani ambalo nina nafasi bora ya kwenda mbinguni? Katika ulimwengu leo, kuna mawazo mengi tofauti, ya jinsi ya kuchagua kanisa. Ukimuuliza mtu sababu ya kukusanyika katika "kanisa alilolichagua" utapata majibu mengi ya kuvutia. Jiulize mwenyewe, "Kwa nini niko hapa? Kwa nini niende katika kanisa lolote?" Watu wengine husema: "Naweza kumwabudu Mungu sawasawa na asili." "Kanisa hili linajisikia vyema kwangu mimi." "Napenda ngoma." "Wazazi wangu waliabudu hapa." "Ni changamfu; naweza kusikia kile ninachokitaka." "Familia yangu watakwenda nami kama nikienda." Kanisa moja huko Lubbock, TX, inamtazamo mzuri kwa nje kwa upande wa mbele: "Eklesia: kanisa lisilo na dini." Tafsiri ya kanisa ni: "Imani katika au hamu ya kuabudu nafsi kuu kuliko sisi wenyewe." Ninahisi kwamba kanisa hili ni sawa na kumbi fulani za muziki. Jibu lako litakuwa ni nini? Jibu sahihi ni lipi? Ni katika kanisa lipi ninapaswa kuokolewa? Kama tukiikubali Biblia kama neno la Mungu lenye uvuvio, labda tunapaswa kumwuliza Yesu, "Ni katika kanisa lipi ninalopaswa kuabudu? Jibu la Kristo ni nini?

Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia, kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Yesu ndiye njia pekee!

Mt. 16:13-18, "*Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wakasema wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmoja wapo wa manabii. Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simon Petro akajibu akasema, Wewe*

ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia heri wewe Simon- Baryona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."

Mawazo ya ufunguzi

Kanisa langu linaonyesha kwamba kutakuwa na makanisa mengine. Milango ya kuzimu haitalishinda na kwamba milango ya kuzimu itayashinda makanisa mengine.

Shetani alimjaribu Kristo: Mt. 4:8-10 ni kifungu kilichozoeleka. Luka 4:5-8 hufanana, lakini kwa mvuto tofauti.

Luka 4:5-8, "*Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa ye yote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako. Yesu akajibu akamwambia, Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako umwabudu yeye peke yake.*"

Haileti maana kufikiria kwamba mmoja wetu ye yote atakuwa na falme za kimwili. Falme za Kiroho, hataivyo ni swala tofauti sana. Ibilisi anaweza akampatia ye yote uwezo huo. Haa! Naweza nikaanzisha kanisa langu mwenyewe, na naweza nikawa na mwongozo wangu binafsi ya kanisa! Naweza nikasema kitu kile kile kama ambayo Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu". Sasa vipi kuhusu milango ya kuzimu? Swali la msingi sana. "Je milango ya kuzimu italishinda kanisa ambalo nimechagua kwa ajili ya familia yangu, watoto wangu?

Katika kanisa ambalo unahudhuria limeonyeshwa katika Biblia?

Rum. 16:1-16 inaonyesha makanisa tofauti na katika msitari wa 16 inatoa mukhutasari: "*Salimianeni kwa busu takatifu.* ***Makanisa yote ya Kristo*** *yawasalimu.*"

Mt. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika* ***kwa jina langu****, nami nipo papo hapo katikati yao.*" Ni vyema sana kuwa naye katikati yetu! Kwa mamlaka yake! Je unakusanyika kwa mamlaka hayo?

Kanisa la Kristo sio ukumbi wa starehe, chama cha siasa, au sehemu ya kushushia watoto wako ili kwamba uweze kufanya cho chote unaloweza kufanya.

Kanisa la Kristo ni nini hasa?

Ni sehemu ambapo waumini wanamwabudu Mungu.

Yoh. 4:23-24, "*Lakini saa inakuja nayo sasa ipo ambayo waabuduo halisi* ***watamwabudu Baba katika roho na kweli****: maana Mungu awatafuta watu kama hao wa mwabudu. Mungu ni Roho nao wa mwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Siyo jengo la kimwili. Ni ufalme wa Kristo wa Kiroho na ni lazima tuwe ndani yake ili tuokolewe. Kuingia katika ufalme wa Kristo lazima tuzaliwe ndani yake.

Yoh. 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambia, Amin, amini, nakuambia,* ***mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu****. Nikodemo akamwambia awezaje kuzaliwa mtu akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye maya ya pili akazaliwa? Yesu akajibu Amini, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Je umewahi kubatizwa (kuzaliwa) katika mwili wa Kristo?

Gal. 3:27-29, "*Maana ninyi nyote* ***mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo****. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke.* ***Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu****. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*"

Efe. 1:19-23, "*Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka katika mkono wake wa kuume katika ulimwengu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Kristo ndiye njia pekee ya kwenda kwa Baba.

Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia kweli na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Yoh. 10:1, "*Yesu aliwaambia, Amin, amin, nawaambieni, Yeye asiyeingia mlangoni katika zizi la kondoo, lakini akwea penginepo, huyo* ***ni mwivi naye ni mnyang'anyi****.*"

Mdo 4:12, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Hataivyo, mwanadamu atajaribu kutafuta njia nyingine mbadala. Yesu anamwita mtu kama huyo mwivi na mnyang'anyi.

Mt. 7:13-23, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni; nao ni wengi waingiao kwa kupitia mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani,* ***nao waionao ni wachache****. Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Viyvo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa na kutupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua. Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali* ***ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni****. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Yesu anaelezae wazi wazi njia pana imejaa na makanisa mengine mengi ambayo hayatambuliwi na Bwana; imejawa na watu wakarimu wanaoongozwa na mbwa mwitu waliovaa mavazi ya kondoo, watakaoshangazwa wakati Kristo atakapowaambia, "Ondokeni, Siwajui." Anawatambua tu wale ambao wapo katika **mwili Wake**.

2 Tim. 2:19, "*Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye mhuri hii, Bwana awajua walio wake, na tena kila alitajaye jina la Bwana na auache uovu.*"

Kanisa ninalopaswa kuabudu inafundisha tu maagizo ya Kristo.

Mk. 7:6-7, "*Akawaambia Isaya alitabiri vyema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, watu hawa hunieshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami; nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*"

Mt. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,* ***mkiwabatiza*** *kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha* ***kuyashika yote*** *niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Kanisa la Kristo linakumbuka dhabihu yake kila siku ya kwanza ya juma.

Mdo. 20:7, "*Kila siku ya kwanza ya juma, mitume walipokutana katika kuumega mkate, Paulo akawahutubu…*"

Yoh. 6:53, "*Yesu akawaambia, Amini, amini, nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu.*"

Mara moja kwa nyakati chache Kristo alitoa agizo la moja kwa moja kwetu ni kukumbuka mauti take katika ushirika wa meza ya Bwana.

Luka 22:19, "*…fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*"

Katika 1 Kor. 11 Paulo anatukumbisha tusisahau dhabihu hii; msitari wa 24, "*…twaeni mle: huu ndiyo mwili wangu, ulio kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*"

Kama hatuchunguzi hii kwa imani, Paulo anatuambia katika mustari wa 30 kwamba tunakuwa wagonjwa na dhaifu kiroho, na mara tunasinzia. Kuchunguza huku ilikuwa ni hatari kwa Kristo na Paulo, na pia inachukuliwa kirahisi katika makanisa mengi na wengine hawashiriki kabisa. Vipi kuhusu kanisa unaloabudu?

Je kanisa ambalo wewe unaabudu ndilo ambalo Kristo atalitoa kwa Baba wakati atakapo kuja tena?

Sasa, uchaguzi wetu wa kanisa inaanza kuwa na maanani zaidi. Inaonekana haipaswi kuchukuliwa kirahisi.

1 Kor. 15:24, "*Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme…*"

Sasa inakuwa muhimu kuwa katika kanisa sahihi badala ya kuwa na yetu sisi wenyewe au kuwa katika kanisa lingine ambalo halijaamuliwa na Kristo. Sababu za kuwa pale zinaonekana wazi. Ahadi ya shetani kuturuhusu kuabudu katika njia ambayo tunaipenda, katika kanisa ambalo tunaitaka, inaonekana kidogo haipendezi. Kuwa katika kanisa la Kristo ni kila kitu.

Kristo anaswali linalovutia katika Luka 6:46, "*Kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, wakati hamtendi yale niwaamuruyo?*" Jibu lako ni nini?

Jibu la Kristo linapatikana kataka sehemu iliyobaki ya kifungu hiki. Mistari ya 47-49, "*Kila mtu ajye kwangu na kuyasikia maneno yangu na kuyatenda, nitawaonyesha mfano wake. Mfano wake ni mtu ajengaye nyumba, na kuchimba chini sana, na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika, mto uliishukia nyumba ile kwa nguvu, usiweze kutikisika; kwa kuwa imejengwa vizuri. Lakini yule aliyesikia wala hakutenda, mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi, pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu, ikaanguka mara; na maangamizi yake nyumba ile yakawa makubwa.*"

Tunahatarisha kila kitu na kila mmoja ambao wanathamani kwetu tunapoabudu katika kanisa ambalo halijajengwa na Kristo.